بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Pakistan

Jumatatu, 9 Shawwal 1446 H | 07/04/2025 M | Na: 36 / 1446

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## Farauni wa Washington Afanya Maangamizu Makubwa Gaza, Kwa Usaidizi Kamili wa Viongozi wa Kijeshi na Kisiasa wa Waislamu na Mayahudi.

**Jibu Pekee la Kisharia ni Uhamasishaji wa Majeshi ya Waislamu. Enyi Waislamu! Songeni kwa ajili ya Faradhi ya Kisharia!**

**(Imetafsiriwa)**

Bila jeshi hata moja la Waislamu kumzuia, Trump alitimiza ahadi yake ya kufanya maangamizi makubwa Gaza. Kamera zimenasa picha za sehemu za miili ya waumini zikipaa angani, juu ya majengo marefu, kutokana na kukithiri kwa mashambulizi ya makombora. Madaktari wa uokoaji wanafunikwa macho na kupigwa risasi. Watoto, wanawake, wazee na waliojeruhiwa wanauawa shahidi kwa kulipuliwa mahema yao. Sera ya njaa ya Amerika, iliyotekelezwa na wafuasi wake, umbile la Kiyahudi, imeongeza mateso hadi kiwango cha baa la njaa. Sasa imedhihirika kwa kila mtu kwamba Firauni wa Washington anafanya maangamizi makubwa kwa Gaza, kwa usaidizi kamili wa kijeshi na uongozi wa kisiasa wa Waislamu na Mayahudi. Enyi Umma wa Muhammad (saw)! Chukueni tahadhari ya Muhammad al-Mustafah (saw) ya Mwenyezi Mungu kututelekeza, pindi tunapowatelekeza Waislamu!

«مَا مِنَ امْرِئٍ يَخْذُلُ امْرَأً مُسْلِماً فِي مَوْضِعٍ تُنْتَهَكُ فِيهِ حُرْمَتُهُ وَيُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ، إِلَّا خَذَلَهُ اللهُ فِي مَوَاطِنَ يُحِبُّ فِيهَا نُصْرَتَهُ»

**"Hakuna Muislamu atakayemtelekeza Muislamu mwengine mahali ambapo utukufu wake unakiukwa na heshima kuvunjwa isipokuwa Mwenyezi Mungu atamtelekeza mahali ambapo angependa nusra yake."** (Abu Dawud)

Kwa kuhisi uchungu mkubwa wa Gaza, Ummah uko katika hali ya unyonge na kuchanganyikiwa, ambayo inasababisha baadhi ya vitendo visivyo na athari. Fauka ya hayo, hisia za majuto na aibu ndani ya Ummah kwa kutoweza kuwanusuru Waislamu wa Gaza kwa hakika ni matokeo ya kutokuwepo mpango kazi wa wazi. Hizb ut Tahrir/Wilayah Pakistan inawasilisha nukta nne zifuatazo kwa Waislamu ili maumivu yetu na juhudi zetu za kisiasa zifikie matokeo yanayoonekana kivitendo kwa mujibu wa faradhi ya Shariah.

**Kwanza:** Waislamu lazima wawajibishe viongozi wao wa kijeshi na kisiasa kuhusu suala la Gaza. Nchini Jordan, Syria, Mauritania, Algeria, Morocco na maeneo mengine, Ummah unayataka majeshi kuhamasishwa kwa ajili ya jihad. Kumhisabu mtawala ni faradhi ya Shariah. Ni lazima tutake kwamba uongozi wa kisiasa na kijeshi wa Pakistan utume vikosi vya jeshi kuwanusuru Waislamu mjini Gaza. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

« كَلَّا، وَاللَّه لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ، وَلَتَنْهَوُنَّ عَنِ الْمُنْكَرِ، ولتَأْخُذُنَّ عَلَى يَدِ الظَّالِمِ، ولَتَأْطِرُنَّهُ عَلَى الْحَقِّ أَطْرًا، ولَتَقْصُرُنَّهُ عَلَى الْحَقِّ قَصْرًا، أَوْ لَيَضْرِبَنَّ اللَّه بقُلُوبِ بَعْضِكُمْ عَلَى بَعْضٍ، ثُمَّ ليَلْعَنَكُمْ كَمَا لَعَنَهُمْ»

**"Hapana, Naapa kwa Mwenyezi Mungu mtaamrisha mema na mtakataza maovu na mtaukamata mkono wa dhalimu na mtamshawishi atende uadilifu na kushikamana na haki, au Mwenyezi Mungu atazingonganisha nyoyo zenu nyinyi kwa nyinyi na atakulaani kama alivyowalaani."** (Imeorodheshwa kama Hassan na Abu Daawuud na At-Tirmidhiy).

**Pili:** Matakwa makubwa ya umma ya uhamasishaji wa vikosi vya jeshi, kwa kutumia mitindo kama vile maandamano, taarifa kwa vyombo vya habari, khutba kutoka kwenye minbari za misikiti, mabango, vibandiko na mikusanyiko. Vyama vya biashara na viwanda, mabaraza ya wanasheria, vyama vya wafanyibiashara, mashirika ya wanafunzi, vyama vya kisiasa, vyama vya wanataaluma, vyama vya waandishi wa habari, kamati za maulamaa na miundo mingine yote ya pamoja ndani ya wenye ushawishi mkubwa lazima ipaze sauti zao na kutaka kuhamasishwa kwa vikosi vya jeshi vya Waislamu ili kuinusuru Gaza.

**Tatu:** Kila mtu kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii lazima atoe wito wa kuhamasishwa kwa majeshi ya Waislamu kuinusuru Gaza. wanapodi wanapaswa kufanya vipindi juu yake, watu wanapaswa kuweka mbele matakwa ya uhamasishaji wa majeshi kwa njia ya video, sauti na maandishi.

**Nne:** Waislamu lazima wawatembelee jamaa zao, marafiki na majirani, maafisa wa kijeshi ndani ya duru zao za asili, wawakilishi wa vyama vya kisiasa, makhatibu katika misikiti, maulamaa, na kila mtu mwenye ushawishi, kibinafsi na katika mikusanyiko, na kuwataka watumie uwezo wao wote, nguvu zao, na ushawishi ili kuhamasisha majeshi yetu kuelekea Gaza. Na ni juu ya Umma kuwakumbusha neno hili la Mwenyezi Mungu,

**[وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا وَاجْعَلْ لَنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيّاً وَاجْعَلْ لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيراً]**

**"Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako"** [Surah An-Nisa, 4:75].

**Enyi Waislamu!** Inukeni na muinuke kutoka katika hali yenu ya unyonge na kuchanganyikiwa. Tangu mwanzo, lilikuwepo suluhisho moja tu la Sharia kwa tatizo la Gaza. Ni faradhi ya Sharia kwa ajili ya kuhamasishwa kwa majeshi ya Waislamu katika Jihad. Tumieni ushawishi wenu kuhakikisha suluhisho hili la kina la Shariah, kwa kuwanusuru Waislamu waliodhulumiwa wa Gaza na Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina!

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Pakistan**

**Tovuti:** www.hizb-pakistan.com http://HizbPK.page.tl
**Pepe:** HTmediaPAK@gmail.com **WhatsApp: +90-531-814-7385**
**Twitter**: http://Twitter.com/HTmediaPAK **Facebook:** https://Facebook.com/HTmediaPAK10
**YouTube**: http://YouTube.com/HTmediaPAK **Dailymotion:** https://Dailymotion.com/HTmediaPAK

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info